



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MLIMBA



**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA ROBO YA KWANZA CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 03/11/2021 KILICHOKETI OFISI YA AFISA ELIMU (W)**

**MAHUDHURIO**

- |                           |            |
|---------------------------|------------|
| 1. Witness R.Kimoleta     | Mwenyekiti |
| 2. Suleiman Maseko        | Katibu     |
| 3. Colex A. Mwakyelu      | Mjumbe     |
| 4. Joseph E. Mgana        | Mjumbe     |
| 5. Dr Christina L. Guveti | Mjumbe     |
| 6. Elias M. Malinjanga    | Mjumbe     |
| 7. Wakili, Nakua F.A      | Mjumbe     |

**SEKRETARIETI**

1. EUNICE Y. MHILU
2. IPYANA J. MWANSASU

**MUHTASARI NA. TB/01/11/2021 – KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alimkaribisha mwenyekiti, Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe kwa kuwasihi kupitia taarifa zilizowasilishwa kwa makini ili kutoa maamuzi sahihi na kufungua kikao mnamo saa 10:30 Jioni .

**MUHTASARI NA. TB/02/11/2021 – KURIDHIA AJENDA**

Ajenda saba(7) ziliwasilishwa. Wajumbe walipokea na kuridhia agenda hizo ziwe mwongozo wa kikao.

Ajenda hizo ni;

1. Kufungua kikao
2. Kuridhia Ajenda

3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha bodi ya zabuni cha tarehe 28/05/2021
4. Kuidhinisha manunuzi ya vifaa na huduma mbalimbali kwa Idara na Vitengo
5. Utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19
6. Mengineyo
7. Kufunga kikao

**MUHTASARI NA. TB/03/11/2021 – KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI CHA TAREHE 28/05/2021.**

- Wajumbe wa bodi ya zabuni walipitia muhtasari wa kikao cha 28/05/2021 na kuuridhia baada ya marekebisho machache yakiuandishi kufanyika na kuagiza mambo yafuatayo majibu yake yawasilishwa kwenye kikao kinachofuata;-
  - Circural iwepo kwenye makablasha ili wakati wa kikao wajumbe waweze kutambua manunuzi yaliyofanyika

**MUHTASARI NA. TB/04/11/2021 – KUIDHINISHA MANUNUZI YA VIFAA NA HUDUMA MBALIMBALI KWA IDARA NA VITENGO**

Bodi ya zabuni ilipokea na kupitia taarifa ya timu ya tathmini kwa ajili ya kupitisha vifaa vya Umaliziaji wa majengo manne ujenzi wa hospitali ya Wilaya ambapo;-

- Bodi ya zabuni imetunuku zabuni za vifaa vya umaliziaji hatua ya kufunga gata,dari,sakafu na rangi majengo manne apewe mzabuni **Sebastian M Ngoda** kwa kiasi cha Tsh **112,304,500/=**.
- Bodi ya zabuni imetunuku zabuni za vifaa vya umeme awamu ya pili majengo manne apewe mzabuni **Petronila Electrical Supply** kwa kiasi cha Tsh **57,129,100/=**.
- Bodi ya zabuni imetunuku zabuni ya vifaa vya umaliziaji awamu ya pili vifaa vya mfumo wa maji safi na maji taka majengo manne apewe **Jakems Investment LTD** kwa kiasi cha Tsh **47,413,600/=**.

Baada ya bodi kutunuku zabuni tajwa hapo juu iliagiza uwasilishwaji wa taarifa za tathmini uwe ni wa kupitia kikao cha manunuzi ambacho kitafanya ufupisho wa taarifa iyo na kuagiza vifaa vinunuliwe kwa awamu kulingana na vipaumbele na uhitaji.

**MUHTASARI NA. TB/05/11/2021 – UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO-19**

Kuridhia kukasimisha mchakato wa manunuzi madaraka au kamati kwa ajili ya kusimamia taratibu zote za ujenzi wa madarasa ya UVIKO 19

Baada ya bodi ya zabuni kupokea taarifa ya mapokezi ya fedha za UVIKO 19 wajumbe waliridhia kukasimisha majukumu ya usimamizi kwa bodi za shule kwa ajili ya kusimamia taratibu zote za ujenzi wa madarasa ya UVIKO 19.

Bodi imesisitiza mambo yafuatayo yazingatiwe;-

- Ujenzi uzingatiwe viwango na ukaguzi wa wataalamu kabla ya malipo
- Manunuzi yote yazingatie taratibu za manunuzi ili thamani ya fedha iweze kuonekana

Bodi ya zabuni iliagiza barua ya maelekezo iwasilishwe kwa wajumbe ili waweze kuipitia.

#### **MUHTASARI NA. TB/06/11/2021 – MENGINEYO**

- Bodi imekubaliana kuwa manunuzi ya vifaa vya ujenzi wa miradi yawasilishwe kwenye vikao vya bodi kuliko kutumia circular.
- Bajeti iandaliwe kwa kuzingatia vikao vya dharura na chakula

#### **MUHTASARI NA. TB/07/11/2021 – KUFUNGA KIKAO**

Baada ya ajenda zote kujadiliwa Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao na kufunga kikao saa 11:54 jioni.


UMETHIBITISHWA



KATIBU



MWENYEKITI



TAREHE